

Manufaa ya kilimo cha maboga

'Ni chakula, na gharama za ulimaji wake ni nafuu'

**Na: Mwandishi wa
Ukulima wa Kisasa**

MABOGA ni zao la chakula ambalo hulimwa katika sehemu nyingi nchini Tanzania, lakini kwa kiasi kidogokidogo sana, aghalabu huwa linapandwa katika mashamba ya mahindi.

Maboga huliwa baada ya kupikwa, na majani yake machanga hipukwa na kutumiwa kama mboga. Katika nchi za Ulaya maboga hutumiwa katika chakula kiitwacho 'pumkin pie'

Twaweza kusema kuwa maboga ni mojawapo ya mazao ya chakula aina bayo yanastahili kulimwa kwa wingi (katika mashamba makubwa); na ni zao ambalo linawezza kuuzwa sokoni.

Wataalam wa kilimo wana-sema kuwa zao hilli linawezza kusitawi katika sehemu nyingi nchini, kuanzia mwambao wa pwani hadi sehemu za bara katika mwinuko wa meta 1,300 kutoka usawa wa bahari.

Kuna alia nyingi za maboga, ambazo zinatofautiana kwa umbile, ukubwa, na rangi. Hata hivyo, aina zinazoonekana kwa wingi nchini ni panoja na Flat Boer, Queensland Blue, na Green Hubbard.

Mkulima akitaka kulima zao hilli katika shamba kubwa itampasa kutafuta mbegu za aina ya maboga anayoipenda. Mbegu hizo azipande shambani kwa nafasi ya sentimetra 60 kutoka shimo hadi shimo jingine, na sentimetra 110 kutoka safu hadi safu nyingine. Katika kila shimo apande mbegu 2 au 3.

Miche ikisha kuchipua na kufikia urefu wa sentimita 10 hadi 15, aipunguze idadi yake kwa kung'oa baadhi ya miche na kubakiza miwili-miwili au mmoja-mmoja.

Shamba linahitaji kupaliliwa

mapema magugu yaanzapo kuota, na kazi hii inaweza kufanya kwa safari mbili tu. Tahadhari tchukuliwe ili mimea lisikatwe au kuharibiwa wakati wa kupalilia.

Iwapo udongo hauna rutuba ya kutosha, mkulima yampasa kutia shambani mbolea ya samadi, au mbolea za viwandani za NPK au TSP wakati wa kupanda mbegu.


WADUDU: Mafunza (maggots) yanayozaliwa na inzi waitwao Curcubita Flies, husababisha maboga kuoza. Mkulima anaweza kuwaepuka wadudu hao kwa kunyonyizia dawa ya Malathion wakati mimea ya maboga imeanza kutoa maua.

UGONJWA: Ugonjwa 'uitwao Downy Mildew' husababisha

majani ya maboga kukauka, na wakati mwingine mmea wote unaweza kufa. Mkulima anaweza kuudhibiti ugonjwa huu kwa kunyonyizia dawa ya Dithiocarbamate.

Maboga hukomaa katika muda wa miezi 4 au 5, lakini uchumaji wa majani yake kwa ajili ya mboga unaweza kuanza wakati mimea imeanza kutoa maua.

Baadhi ya maboga huvunwa wakati yameishakomaa kiasi cha kutosha, yaani wakati ngozi yake imekuwa ngumu sana; na maboga mengine huvunwa kabla hayajakomaa sana. Kila mmea una uwezo wa kuzaa maboga 4 au 5, na kila boga linawezza kuwa na uzito wa kilo 2 kwa wastani.



Boga alia ya Flat Boer.

Kutoa bidhaa nje ya nchi siyo rahisi

Na: Alfred Magembe

MKULIMA akitaka kusafirisha bidhaa zake nchi za nje kwa

ajili ya kuuza, atakumbana na matatizo mengi ambayo kila mfanya biashara hupambana nayo, kwani mkulima huyo aki-
(Inaendelea Uk. 13)